LOWELL
PUBLIC SCHOOLS

# Habari Muhimu & Taarifa Mpya Kuhusu Kurejelea kwa Mafunzo ya Kuhudhuria Shule Kibinafsi

**Jadwali la Kurejelea kwa Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi**

• ✓ **Februari 22 -** Wanafunzi katika programu za masomo yaliyo na tofauti kubwa na masomo ya kawaida ambao walikuwa wanashiriki katika muundo wetu wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi (wale wanafunzi ambao bado walikuwa wanahudhuria kibinafsi katika Disemba).

• ✓ **Machi 1 –** Wanafunzi ambao hawamo katika programu za masomo yaliyo na tofauti kubwa na masomo ya kawaida, lakini waliohudumiwa kibinafsi katika majira ya mapukutiko kama mpango wetu wa kiasili wa kufungua shule upya.

• **Aprili 5** – Wanafunzi katika madarasa ya Chekechea hadi 5 watarejea kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kikamilifu, ikiwa na chaguo la mzazi ili mtoto asome kwa mbali kikamilifu.

• **Aprili 26** – Wanafunzi katika madarasa ya 6-8 watarejea kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kikamilifu, ikiwa na chaguo la mzazi ili mtoto asome kwa mbali kikamilifu.

• **Aprili 26** – Muundo wa kuchanganya masomo ya mbali na ya kuhudhuria kibinafsi katika LHS ambayo inaisha wakati wa chakula cha mchana. (Jimbo bado inakamilisha mwongozo kwa shule ya upili. Huku tukiongoja mwongozo zaidi wa kudhibiti kutoka DESE (Idara ya Elimu ya Msingi na ya Upili), Wilaya inaendelea kupanga muundo wa kuchanganya masomo, ikitumia jadwali yenye mzunguko ama kushuka. Hii inafanyika ili kurahisisha changamoto za kipekee za kiasi cha wanafunzi na kukuza uendelevu katika Lowell High.)

• **Shule ya Awali –** Wanafunzi wa shule ya awali ambao wamepangiwa kuhudhuria katika Cardinal O'Connell Early Learning Center ambao kwa sasa husoma kwa mbali wanaweza kurejelea masomo ya kuhudhuria kibinafsi kuanzia Aprili 5. Wanafunzi wa shule ya awali wanaosoma kwa mbali katika shule zote zingine wataendelea kusoma kwa mbali kwa wakati huu. Baada ya kurejea kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kwa madarasa ya Chekechea hadi 5 katika Aprili 5, LPS itatathmini upya vifaa vya shule ili kuamua iwapo mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kwa wanafunzi wa shule ya awali itaweza kufanyika katika mashule zingine pamoja na Cardinal.

---

**Kupanua Baraza la Jamii la Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi**

LPS iliandaa mikutano ya mbali ya kuarifu ili kuangazia taarifa mpya kuhusu mpango wa Wilaya kwa kupanua mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi katika mwezi wa Aprili. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu mpango, tafadhali tazama picha na videyo kutoka mikutano haya ya kuarifu:

- Uwasilishaji wa Slaidi wa Upanuzi wa Baraza la Jamii la Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi

- Videyo kutoka mkutano wa Machi 16

---

**Usafirishaji kwa Wanafunzi wa Kuhudhuria Kibinafsi**
Tumeweza kupanua kwa usalama huduma yetu ya usafirishaji bila kusongamana katika mabasi na sasa tunaweza kuwapatia basi wanafunzi katika madarasa ya Chekechea hadi 8 wanaoishi angalau maili 1.75 kutoka shule yao.

Familia ya wanafunzi wanaorejelea mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi mnamo Aprili 5 walitumia baruapepe iliyo na taarifa maalum kuhusu jadwali la basi ya mtoto wao, ikiwamo mahali pa kumchukua na kumweka mtoto. Wanafunzi wa Chekechea na darasa la kwanza watapokea pasi za kimwili za basi. Pasi za basi zilitumwa hapo awali wiki hii. Wanafunzi katika madarasa ya 2-5 hawatapokea pasi za basi na watapokea taarifa ya basi yao kupitia baruapepe.

Taarifa ya basi inaweza kupatikana pia kwa kubonyeza ikoni ya basi katika ukurasa ya kwanza ya tovuti la Lowell Public Schools. Utahitaji nambari ya kitambulisho ya mwanafunzi ili kupata taarifa hii. Hii ni nambari yenye tarakimu 6 ambayo mtoto wako hutumia kuingia katika kompyuta yake ya shule.

Tutakuwa tukituma taarifa kuhusu usafirishaji wa basi kwa wanafunzi katika madarasa ya 6-8 katika wiki ya Aprili 12.

Iwapo una maswali yeyote, tafadhali wasiliana na shule yako, au pigia Ofisi ya Usafirishaji ukupitia 978-674-4333.

---

**Huduma ya Chakula kwa Wanafunzi wanaosomea kwa Mbali**

Kuanzia Jumatatu, Aprili 5, tutakuwa tunahamia kwa jadwali hii ifuatayo kwa wanafunzi wanaosoma kwa mbali:
Sehemu zifuatazo zitakuwa zikitoa huduma ya chakula ya kila siku kwa wanafunzi wetu wa kusoma kwa mbali:

- STEM Academy: 11 asubuhi - 1 jioni

Sehemu zifuatazo zitakuwa zikitoa huduma ya chakula kila Jumatatu, kila Jumatano na kila Ijumaa kwa wanafunzi wetu wa kusoma kwa mbali:

- Lowell High: 8 asubuhi - 9 asubuhi
- Morey: 11 asubuhi - 12 jioni
- Robinson: 11:30 asubuhi - 12:30 jioni
- Butler: 12 jioni - 1 jioni
- Wang: 12 jioni - 1 jioni
- Murkland: 12:30 jioni - 1 jioni
- Lincoln: 1 jioni - 1:30 jioni
- Greenhalge: 2:30 jioni - 3 jioni
- Stoklosa: 3:15 jioni - 4 jioni

Wanafunzi watapokea kiamsha kinywa mbili na chakula cha mchana mbili kila Jumatatu na kila Jumatano katika sehemu hizi.
Wanafunzi pia watapokea vyakula kwa siku za wikendi kila Ijumaa katika sehemu zetu zote za chakula.

---

**Data ya COVID-19**

Data ya mwisho kabisa ya COVID-19, taarifa mpya na habari inaweza kupatikana katika Dashibodi ya LPS ya COVID-19. Tafadhali cheki rasilimali hii muhimu ya taarifa. Ripoti ya mwisho kabisa ya ufuatiliaji wa COVID-19 inaweza kupatikana hapa

---

**Programu ya Kipimo cha COVID-19**

Kama sehemu ya mchakato wa kufungua upya wa shule, tumekuwa tukitoa fursa ya kipimo cha hiari cha kila wiki cha COVID-19. Kipimo hiki kitapunguza hatari ya usambazaji wa COVID-19 kwa kusaidia kutambua watu walio na maradhi lakini hawaonyeshi madalili yeyote ya COVID-19. Ili kushiriki, wazazi/walezi wanafaa kutia saini ya idhini kwa mtoto wao. Bonyeza hapa kwa fomu ya idhini.

Kipimo hiki cha COVID-19 ni ya haraka, rahisi na haiumizi. Ni kipimo cha pua ambacho hufuta kwa polepole sehemu la chini la tundu la pua. Tutawarahisishia mahitaji ya wanafunzi wote ili kuwasaidia wafanye kipimo wakiwa na raha.

Kipimo hiki ni cha bure. Hutakiwi kulipia kipimo hiki au kuwa na bima ili kupata kipimo hiki.

Idadi zaidi ya wanafunzi na wafanyikazi wanaoshiriki, itafanya shule zetu kuwa salama zaidi. Tafadhali bonyeza hapa ili kusoma zaidi kuhusu programu ya kipimo.

---

**Chanjo la COVID-19**
Massachusetts sasa iko katika awamu ya pili ya kutoa kwa chanjo ya COVID-19, ambayo sasa inajumuisha wafanyikazi wa chekechea hadi madarasa ya 12. Wengi wa wafanyikazi wetu wamepewa chanjo ama wamo katika mchakato wa kupokea kipimo chao cha kwanza au cha pili cha chanjo. Kwa taarifa zaidi kuhusu chanjo la COVID-19 na kuona ni lini unaweza kustahiki kupokea chanjo, tembelea tovuti la jimbo.
Pia, tazama rasilimali hizi zenye usaidizi kutoka Lowell Community Health Center (Kituo cha Afya cha Jamii cha Lowell) na Greater Lowell Health Alliance (Muungano wa Lowell Pana ya Afya):

- Jua ni Mambo Gani ni Ukweli na Gani ni Uwongo Kuhusu Chanjo za COVID-19
- Sasa tuna chanjo mbili za kutulinda kutokana na COVID-19 - Haya ndiyo unayofaa kujua

---

**Itifaki na Miongozo ya Barakoa ya Uso ya LPS**
Wanafunzi, wafanyikazi, na mtu yeyote anayeingia shule zetu anatakiwa kuvaa kifunika uso, isipokuwa kama kuna sababu ya kipekee ambayo ina ushahidi wa barua. Barakoa zinaweza kupunguza kasi ya virusi na inaweza kulinda dhidi ya usambazaji wa virusi kutoka watu ambao wanaweza kuwa virusi na wanaweza kuwa hawaonyeshi madalili. Tafadhali rejelea Itifaki na Miongozo ya Barakoa ya Uso ya LPS.

---

**Miongozo ya Umbali wa Kijamii**
The Massachusetts Department of Elementary and Secondary Education (Idara ya Massachusetts ya Elimu ya Msingi na ya Upili) (DESE) imetoa miongozo mapya kuhusu umbali wa kijamii ulio na msingi na maoni ya mwisho kabisa kutoka jamii ya afya na hii itabadilisha kikubwa namna umbali wa kijamii katika madarasa ya LPS yatapimwa kuendelea mbele. Hapo awali, kulingana na mpango wetu wa awali wa kufungua upya, umbali wa kijamii uliwekwa kuwa angalau futi 6 kwa wanafunzi wote. Kuanzia Aprili 5, masharti ya umbali wa kijamii yatabadilika kuwa angalau futi 3. Inapowezekana, tutajaribu kuweka zaidi ya futi 3 inayohitajika.

---

**Itifaki za Usafishaji wa COVID-19**
Huku wanafunzi wakirejelea shuleni, tutaendelea kufuata madhubuti miongozo ya usalama ili kuendelea kulinda wanafunzi na wafanyikazi wetu. Vifaa vya kusafisha hewa vitaangaliwa kuhakikisha vinafanya kazi inavyohitajika, vituo vya kusafisha mikono kuua virusi na vifaa vya darasani vya kusafisha mikono vitajazwa, na madawati pamoja na sehemu zote zitasafishwa kila mara.
Wafanyikazi wetu wa usafi wataendelea kusafisha shule kuondoa virusi, wakitumia vifaa kama vifaa vya kuua virusi/vinyunyizi, haswa mtu aliye na maradhi ya COVID akitambuliwa.

---

**Unachofaa Kufanya Unapokuwa Mgonjwa**
Je unasikia vibaya au unazo dalili za COVID-19? Tafadhali rejelea cheti hiki chenye usaidizi na ambacho ni rahisi kufuata kwa miongozo kuhusu iwapo unafaa kuenda shule na muda gani unafaa kujitenga au kuingia karantini iwapo una dalili au umo katika hatari ya kusambaziwa COVID-19. Tafadhali hakikisha umewasiliana na muuguzi wa shule yako iwapo mtoto atadhihirisha dalili za COVID au iwapo ametambuliwa kuwa mtu wa karibu wa mgonjwa au iwapo alipatikana na maradhi ya COVID.